Toleo 45

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## TAFUTENI KWANZA

Katika maisha yetu kila siku tunafanya maamuzi na uchaguzi wa aina tofauti tofauti. Nitafanya nini? Niseme nini? Nitende nini? Nitatumia vipi wakati wangu, nguvu zangu, na pesa zangu? Nayo mioyo ya wanadamu hujulikana hali yake halisi kupitia kwa maamuzi ambayo wanayofanya, haijalishi maneno wanayosema au kuyadai. Maamuzi yetu ndio hudhihirisha mambo tunayotilia maanani maishani mwetu. Watu wa dunia huzingatia mambo ya kujifurahisha, kutafuta pesa, kujulikana, faraja za maisha, n.k. Naye Yesu katika Hotuba ya Mlimani alitwambia "Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33).

Kama Wakristo tunahitaji kuweka nambari moja na kutilia kipa umbele mambo ambayo yanahusiana na Mungu—zaidi ya mambo mengine yote. Ukweli kwamba wengi tunaloliitia jina la Kristo tunatafuta mambo ya ulimwengu huu ni jambo la kuhuzunisha sana. Wengi wetu hatuweki mambo ya Mungu kuwa nambari moja. Lakini maisha ya Wakristo yanahitaji kupata maana na kutambulika kwa jinsi wao wanamtafuta Kristo na utakatifu wake.

Kusema kweli kuna mambo ambayo ni lazima tuyatafute maishani. Tunahitaji chakula na nguo, na pia ni muhimu sisi kutumia wakati wetu na familia zetu, na tena kupata muda wa kulala na kufanya kazi. Lakini pia ni kweli kwamba Bwana wetu Yesu, kabla ya kufundisha kuhusu kutafuta ufalme wa Mungu, alitambua umuhimu wa mambo hayo ya kawaida. "Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini? Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote" (Mathayo 6:31-32). Basi Yesu hakuwa anafundisha kwamba tuyapuuze mambo hayo, bali alikuwa akifundisha kwamba tusisumbuke kwa ajili ya mambo hayo, kwa maana Mungu anajua mahitaji yetu na Yeye atakutana nayo. Alikuwa akitoa mwito kwa wafuasi wake kwamba wamfanye Mungu kuwa nambari moja maishani mwao, na kuweka mambo ya Bwana kuwa ya muhimu zaidi kuliko mambo mengine yote. Ndipo hapo akaahidi kwamba "hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33b).

Ili Mkristo aweze kupata furaha na ushindi wa kweli katika utumishi wake kwa Mungu, anahitaji kuyapa mambo ya Bwana kipa umbele. Sio makosa sisi kuwa na maono, mipango, na malengo, lakini mambo hayo yote yanahitaji kuwekwa wakfu kwa Mungu, na hata wakati mwingine yawekwe kando ili Mungu apewe umuhimu zaidi. Hakuna cha muhimu zaidi kuliko nafsi zetu ambazo zitadumu milele, ndiposa tunahitaji kuweka umuhimu kabisa kwa swala la utunzaji wa nafsi zetu, zaidi ya mambo yote ya ulimwengu.




"Nayo mioyo ya wanadamu hujulikana hali yake halisi kupitia kwa maamuzi ambayo wanayofanya, haijalishi maneno wanayosema au kuyadai."

Katika maamuzi yote tutakayofanya tuna jukumu la kujiuliza, "Je, mimi ninamweka Mungu kwanza katika jambo hili?" Badala yake Wakristo wengi wanatoa vijisababu na kuleta ubishi kwa ajili ya uchaguzi na maamuzi yao, kwa kutumia visingizio ambavyo Yesu mwenyewe alivimulika katika Luka 14:16-20. Wengine hutoa visingizio vya ukosefu wao wa kujitoa kikamilifu kwa mambo ya Mungu kwa kusema: kuna mali yangu ambayo nahitaji kwenda kujua mahali iko, nina ng'ombe zangu ambazo nahitaji kuhakikisha zilivyo, au mimi nimeoa mke majuzi tu. Wakati ambapo orodha hiyo inazidi kuongezewa, swali kubwa ni: Je, Mungu ndiye nambari moja maishani mwako? Je, maamuzi yako yanaonyesha ukweli huo?

Mambo ambayo ni halali na pia sio dhambi wakati mwingi huchukua muda wetu na kuteka akili zetu. Lakini Wakristo wanahitaji kumweka Mungu juu ya mambo hayo ambayo

*(Endelea katika Ukurasa 2)*


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Tafuteni Kwanza | Tahariri | Mwongozo wa Kujifunza Biblia: Funguo za Mkristo Mpya | Funguo za Kumsaidia Mkristo Mpya | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
| 1 | 3 | 4 | 5-7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

ni halali, kwa maana yao huwa kama mtego, na ndio ambayo yatafinya na kutoa nje tunda la roho kutoka ndani mwetu, kama sisi hatuwi waangalifu. Ndiposa Yesu alitwambia "Basi, jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na . . . masumbufu ya maisha haya . . . kwa kuwa ndivyo itakavyowajilia watu wote wakaao juu ya uso wa dunia nzima." (Luka 21:34-35).

Je, sisi tunamtafuta Mungu kwanza au tunaweka umuhimu kwa mambo yanayoonekana kuwa ni halali? Tunahitaji kumtafuta Mungu kwanza na kumruhusu Yesu atuongoze kuchagua tutaishi wapi, tutamwoa nani, na ni kazi ipi tutafanya. Mambo haya ambayo ni halali yanahitaji kuwekwa nambari ya pili. Lakini wengi wetu tunatafuta utajiri wa ulimwengu. Na ingawa sio vibaya mtu kuwa na pesa, ni makosa kufanya utafutaji wa pesa uwe ndio nambari moja, huku tukiyafanya mambo ya Mungu kuwa nambari ya pili.

Wakati Wakristo wanautafuta kwanza ufalme wa Mungu, wao humpatia Mungu wakati wao ambao unafaa zaidi, pesa zao, na vipawa vyao. Mkristo anahitaji kuwa na muda fulani kila siku wa kusoma Biblia na kuomba. Lakini tukipuuzilia mbali mambo haya mawili, hii ni kumaanisha kwamba kuna mambo mengine tuliyoyapatia kipa umbele. Je, sisi tunahudhuria nyakati za ibada na ushirika na Wakristo wale wengine? Je, tunautafuta kwanza ufalme wa Mungu? Je, ni nini ambacho kinachukua nafasi ya kwanza maishani mwetu wakati kuna mahitaji katika kazi ya Mungu, ilhali tunatumia pesa zetu kujifurahisha, au kuhifadhi pesa zetu kwa ajili ya siku za usoni, na tunakosa kupeana fedha hizo kwa huduma ya Mungu kwa njia ya kujitolea?

Mambo ambayo Mkristo wa kweli hutilia umuhimu ni tofauti kabisa na yale yanayotiliwa umuhimu na watu wa ulimwengu. Mtume Paulo alifundisha kusanyiko la Wakristo wa Roma na kusema: "Msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:2). Basi kizazi hiki cha sasa kinahitaji kufanya upya mawazo yao ili kiweze kuelewa kwamba kutafuta ufalme wa Mungu sio tu matamshi ya kithiolojia tunayosema; bali ni ukweli halisi. ■

Kuna gharama tunahitaji kulipa ya kumweka Mungu nambari ya kwanza, na mambo ya ulimwengu kuwa nambari ya pili, lakini malipo tutakayopata kwa kujinyima kwetu kutatuletea malipo yanayostahili kabisa.



USIMUULIZE MTU KILICHO MUHIMU KWAKE.

TAZAMA TU JINSI ANAVYOTUMIA WAKATI WAKE.

-Dale Carnegie

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo.* — Waefeso 4:15

Ni jambo la utukufu kuona mtu amebadilishwa kabisa na Yesu. Na ni jambo la kufurahisha sana kupata watoto wapya wa kiroho katika mwili wa Kristo. Waumini wapya huleta uhai na ari mpya kati ya watu wa Mungu, na kazi ya kuwatunza pamoja na uwepo wao hupatia ibada na ushirika uhai mpya. Lakini lengo letu kamili linastahili kuwa sio tu kuongezea watoto wapya wa kiroho, bali pia kwamba watoto waliozaliwa hapo mbeleni waweze kukua ndani yake Kristo. Bwana anataka waumini wapya kuendelea kukua kiroho hadi kufikia uwezo wa wao kuwa gunzo katika Kanisa la Mungu.

Ni jambo la huzuni kwamba waumini wengi wapya huishi katika hali ya udhaifu, na pia inahuzunisha kwamba watoto wa kiroho wapya wanaorudi nyuma ni wengi mno. Lakini jambo hili halistahili kuwa hivyo, Mungu ametupatia vyakula vyote vya kiroho na utunzi kwa ajili ya kukua kwa Wakristo wapya. Lakini waokovu wengi wapya hurudi nyuma au kukua kwao kama Wakristo kunalemazwa, jambo ambalo si lazima liwe hivyo. Wakristo wapya hawahitaji kuhofu kwamba hawataweza kuishi maisha ya ushindi kwa Mungu. Kuna baraka nyingi na ushindi kwa kila mmoja ambaye atakubali ushauri na kufuata mpango wake Mungu.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Lengo la toleo hili ni kushiriki baadhi ya funguo za kuwasaidia Wakristo wapya ili wao wazitumie kudumisha maisha yao na kukua kiroho. Hata ingawa funguo hizi zinalenga Wakristo wapya, matumizi ya funguo hizi pia huwawezesha Wakristo waliokomaa kuendelea kukua na kufanikiwa. Mungu atafanya sehemu yake kuhakikisha kwamba tumepata ushindi, lakini kamwe hatuwezi kutokuwa makini na kuishi maisha ya raha mustarehe. Tunahitaji kuwa waaminifu na kufanya maamuzi yanayofaa ili tutoe nafasi kwa makusudi ya Mungu kukamilika ndani yetu. Hatuna budi kufanya uhusiano wetu na Mungu uwe nambari moja na tufuatilie kwa mioyo yetu yote mambo ambayo ni ya Mungu.

Mwokovu mpya hana haja ya kulemazwa na mahitaji yake ya kiroho, kwa maana safari ya wokovu ni ya kila siku—hatua kwa hatua, kidogo kidogo. Mungu atatupatia nguvu na kutusaidia kila siku tunapotafuta mapenzi yake maishani mwetu. Unapofika kwenye mlango uliofungwa, wewe hutoa funguo zako na kutafuta ile ambayo inafaa kwa kufungua mlango huo. Kuna funguo nyingi ambazo tunaweza kuchukua na kutumia kama tutakuwa makini kuzitafuta, ndiposa tuzitumie.

Kama wewe ni Mkristo mpya ambaye ameokoka majuzi, hakuna haja ya wewe kufa moyo. Bwana atakusaidi kukua, kuzaa matunda, na kuwa na ushindi unapofanya sehemu yako ya kukua kama Mkristo. "Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana BWANA, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha" (Kumbukumbu 31:6).

Bwana akubariki na akudumishe katika neema yake na utunzi wake.

*Michael W. Smith*

*Julai 2023*

## Tubuni na Mbatizwe (Matendo 2:38)

**Baada ya mtu kuokoka jambo la kwanza anahitaji kutii ni Mkristo huyo mpya kufuata mfano wa Kristo kwa yeye kutumbukizwa majini kwa ubatizo. Ubatizo ni ushuhuda wa kufufuka kwa mtu ndani yake Kristo, na ni ushahidi unaoonekana wa wokovu ulio ndani yake. Biblia imetoa mwongozo kwamba Wakristo wapya wanahitaji kubatizwa muda tu baada ya wao kuokoka.**

**Jambo hili hutilia nguvu ujuzi wao wa kuokoka na ni njia bora ya kukabilia na shaka zinazoletwa na adui yetu.**

**Basi kama wewe umeokoka na bado hujabatizwa, nakuhimiza ubatizwe bila kukawia zaidi.**

Toleo la Injili Nambari 10: Ubatizo



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Funguo za Mkristo Mpya

**Somo la Maandiko:** *Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani.* —Wakolosai 2:6-7

**Muhstasari:** Kuna funguo za kiroho za kuwasaidia Wakristo katika maisha ya kila siku, funguo ambazo zinaweza kuwafungulia Wakristo wapya (na hata wale waliokomaa) milango ya kukua kiroho na kuweza kupata ushindi wa Kikristo. Wakristo wapya wakitumia funguo hizi wataweza kuishi maisha yenye msimamo dhabiti, na pia kuishi maisha ya utauwa.

### I. Kuwa na Lengo Maishani

A. Wakolosai 3:1-2 Yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko.
B. 2 Wakorintho 7:10-11 Angalieni, kujitahidi, shauku.

### II. Simama kwa Imani, Sio kwa Hisia

A. 2 Wakorintho 5:7 Twaenenda kwa imani, si kwa kuona.
B. Waefeso 2:8-9 Wokovu ni kipawa.
C. Warumi 8:1 Hakuna hukumu katika Kristo.

### III. Jenga Uhusiano Wako na Kristo

A. Yohana 15:4-5 Kaeni ndani ya Kristo.
B. Marko 12:30 Penda Mungu na moyo wako wote.

### IV. Mpendeze Mungu Kila Siku

A. Yohana 14:15 Shikeni amri zangu.
B. Waebrania 12:14 Ishi kwa utakatifu.
C. 1 Wakorintho 10:31 Fanya yote kwa utukufu wa Mungu.

### V. Baraka Inayotokana na Neema

A. 2 Petro 3:18 Kua katika neema.
B. Waebrania 4:16 Msaada kutoka kiti cha neema.
C. 2 Wakorintho 12:9 Neema ya Mungu yatosha.

### VI. Punguza Idadi ya Majaribu

A. Mathayo 26:41 Msiingie majaribuni.
B. Warumi 13:14 Msiuangalie mwili.

### VII. Idumishe Dhamira Safi

A. Luka 19:8-9 Lipia ulichochukua.
B. Matendo 24:16 Dumisha dhamira isiyo na hatia.

### VIII. Jifunze Kutoka kwa Biblia

A. 1 Petro 2:2 Litamani Neno.
B. 2 Timotheo 2:15 Jifunze neno la kweli.
C. 2 Timotheo 3:14-17 Kuendelea katika Maandiko.
D. Zaburi 119:105 Biblia hutumulikia njia.

### IX. Omba

A. 1 Wathesalonike 5:17 Omba bila kukoma.
B. Wafilipi 4:6 Haja zenu zijulikane kwa Mungu.
C. 1 Petro 5:7 Mumtwike fadhaa zenu.

### X. Shiriki na Wakristo Wale Wengine

A. Waebrania 10:25 Tusiache kukusanyika pamoja.
B. Wakolosai 3:16 Muhimizane mmoja kwa mwingine.

### XI. Shiriki Ushuhuda Wako

A. Ufunuo 12:11 Kushinda kwa neno la ushuhuda.
B. Warumi 1:16 Usiionee injili aibu.
C. Marko 16:15 Hubiri injili.

### XII. Mtumikie Bwana

A. Waefeso 2:10 Tuishi tukifanya matendo mema.
B. Mathayo 6:19-20 Kujiwekea hazina mbinguni.
C. 1 Wakorintho 14:12 Kutamani karama za roho.
D. Yakobo 2:14-17 Imani isiyo na matendo imekufa.

### XIII. Ya Kwanza Yawekwe Mwanzo

A. Mathayo 6:33 Tafuta kwanza ufalme wa Mungu.
B. Warumi 12:2 Msifuatishe namna ya dunia.

Tamati

*Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.* —Wafilipi 3:13-14

# FUNGUO ZA KUMSAIDIA MKRISTO MPYA



Baada ya kuokoka na kuachana na ulimwengu, Mkristo mpya ataanza kuelewa ukweli halisi wa maisha haya mapya. Adui atajaribu kumzidi Mkristo huyu mpya kwa maswali mengi, shaka na hofu. Lakini kuna funguo za ukweli ambazo zikitumiwa zitamwezesha mwokovu huyo mpya kuendelea kuwa mwaminifu na kuweza kukua katika mambo ya Mungu.

"Mungu hakutuacha bila silaha, lakini kuna mambo ambayo Wakristo wote wanahitaji kufanya ili kudumisha na kukua katika uhusiano wao na Mungu."

## Huko Peke Yako

Kuna ukweli wa Biblia, na kanuni za maisha ya kawaida, na hata miongozo ambayo ni muhimu sana kwa Mkristo mpya. Wokovu ni ujuzi wa ajabu, lakini kama ilivyo kweli kwa mambo yote mema, kuna bidii na kazi ambayo inahitajika ili mtu aweze kudumisha wokovu huo mpya katika Kristo. Mungu hakutuacha bila silaha, lakini kuna mambo ambayo Wakristo wote wanahitaji kufanya ili kudumisha na kukua katika uhusiano wao na Mungu. Wakristo wapya hawajaitwa kuishi maisha ya utakatifu bila msaada kutoka kwa Mungu. Kama utatafuta na kupata funguo zifuatazo za hekima, ambazo miaka nenda rudi zimetumiwa na watoto wa Mungu, siku zako za usoni zitakuwa zenye ufanisi, na utaweza kuishi maisha yaliyobarikiwa ndani yake Kristo. "Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani" (Wakolosai 2:6-7).

## Dumisha Lengo na Maamuzi Uliyofanya

Moyo na shauku ambayo humvuta mwenye dhambi kwa Kristo ili aweze kuokoka inahitaji kudumishwa kwa lengo la kumfuata Yesu. Ulimwengu utajaribu kumvuta Mkristo mpya ili arudi alikotoka, na majaribu ya hapo awali yatavutia mwili wake. Basi ni ufunguo muhimu sana kwamba Mkristo mpya kila siku "(a)yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu" na "kuyafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi." (Wakolosai 3:1-2). Wokovu ni kazi ya kiungu, lakini Mkristo hana budi kufanya uamuzi na kusema kwamba: "Sitarudi duniani tena!" Mtume Paulo aliwakumbusha waumini wapya wa huko Korintho kuhusu lengo lao la mwanzo: "Maana, angalieni, kuhuzunishwa kuko huko kwa jinsi ya Mungu kulitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo" (2 Wakorintho 7:11). Umakini kama huu wa kudumisha lengo la mwanzo ndio utampatia nguvu Mkristo mpya wakati anapopambana na pingamizi pamoja na majaribu.

## Simama kwa Imani, Sio kwa Hisia

Baada ya kufanya ombi na kupata wokovu, siku hiyo ya wokovu itafika tamati, siku nyingine inaingia, na hisia ulizokuwa nazo za furaha kuu ya kuhakikishwa kwamba wewe ni mwana wa Mungu hutaendelea kuzihisi kwa kiwango cha mwanzo tena. Hapo ndipo Wakristo wapya mara nyingi huanza kujiuliza swali kama kwa kweli wameokoka, wakati hisia hizo zimeanza kudidimia. Lakini ufunguo ambao Mkristo anaweza kutumia sasa ni ule wa imani "Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona" (2 Wakorintho 5:7). Hisia nzuri ni kitu cha ajabu, lakini wokovu haulingani na hisia za mtu. Kwa kweli hisia hutujia tena zinaisha, lakini kipawa cha Mungu ni cha hakika. "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu" (Waefeso 2:8). Basi hebu wewe dumisha imani yako kwa damu yake Kristo iliyomwagika kwa ajili yako, na usiweke imani yako katika hisia zako au

*(Endelea katika Ukurasa 6)*




kazi zako binafsi. Haijalishi shaka na hisia unazohisi sasa, ukweli ni kwamba "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu" (Warumi 8:1). Wakati Shetani ameleta tetezi kuhusu wokovu wako, huo ndio wakati bora wa kujiuliza maswali yafuatayo: "Je, nimefanya dhambi? Je, ningali namtumikia Bwana?" Kama hauna dhambi maishani mwako, na ungali una shauku ya kumtumikia Bwana, basi wewe endelea kufurahia kipawa chake Mungu, na umtupilie mbali Ibilisi na lawama zake.

"Kwa kiwango ambacho tunamkaribia Yesu zaidi na zaidi, ndivyo ambavyo tutazidi kuwa kama Yeye. Kusema kweli tunaweza kuzaa matunda, sio kwa shauku na maamuzi yetu, bali kutokana na kushikanishwa na uhusiano huo kati yetu na Kristo."

## Mjue Yesu

Maisha ya Mkristo hayana haja ya kuongozwa na sheria na miongozo mingi, bali kiini cha maisha hayo ni uhusiano kati ya Mkriso na Mungu. Wakati mwingi Wakristo huwa na ushindani ndani yao, huku wakijaribu kufanana zaidi na Kristo, lakini wanashindwa kufaulu katika jambo hilo. Badala yake, juhudi hizi zinahitaji kutumiwa kwa Mkristo kufanya juhudi za kumkaribia Mungu zaidi na zaidi. Katika Yohana 14:4-5 tunaambiwa: "Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote." Kwa kiwango ambacho tunamkaribia Yesu zaidi na zaidi, ndivyo ambavyo tutazidi kuwa kama Yeye. Kusema kweli tunaweza kuzaa matunda, sio kwa shauku na maamuzi yetu, bali kutokana na kushikanishwa na uhusiano huo kati yetu na Kristo. Lakini msingi wa uhusiano huo si woga, bali ni kumpenda Mungu kwa mioyo yetu yote.

## Mpendeze Mungu Kila Siku

Kama watoto wanaompenda Baba yao, tunahitaji kufanya bidii ili kumpendeza na kumtii Mungu. Yesu akasema, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu" (Yohana 14:15). Funguo moja ya kupata ushindi ni kwa njia ya Mkristo kufanya bidii kila siku kumpendeza Mungu. Hii ni kumaanisha kwamba afanye juhudi za kuishi maisha matakatifu na safi, kwa maana haya ndiyo mapenzi ya Baba. Na wakati maswali yanapoibuka ya nini tunahitaji kufanya, fuata tu mawaidha ya mtume Paulo: "Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" (1 Wakorintho 10:31). Wakati tunapofanya mambo ambayo sio ya utukufu wa Mungu, maisha yetu ndani yake Mungu huanza kuzoroteka.

## Tumia Funguo ya Neema

Mungu amewapatia watoto wake funguo ya ajabu ya kutumia wakati wa shida na majaribu. Huu ni ufunguo wa imani. Hizi ni fadhili za Bwana zinazotusaidia wakati ambapo kamwe hatustahili rehema na nguvu zake. Mtume Petro alitwambia kwamba "kueni katika neema" (2 Petro 3:18). Hebu basi tutafute msaada na tukue katika fadhili zake. Wakati kuna mashindano ndani yetu, huu sio wakati bora wa sisi kuwa mbali na Mungu. Badala yake huu ni wakati wa kujifungulia kwake Mungu, ndiposa "tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji" (Waebrania 4:16). Basi usife moyo wewe mtoto wa Mungu wakati ukihisi wewe ni dhaifu, mtu ambaye hana uwezo, kwa sababu, "Neema yake Mungu inakutosha" (2 Wakorintho 12:9), na nguvu zake zitadhihirika kupitia kwa udhaifu wako wakati ukimtumaini Yeye. Ni baraka kuu kuwa na rasilmali hii ya neema ambayo kamwe haikauki.

## Punguza Idadi ya Mjaribu

Wakati tungali hapa duniani hatuna budi kupatwa na majaribu. Hakuna ujuzi wa wokovu ambao utaondoa misukumo yote na adhari za dhambi katika mwili wa Mkristo. Lakini hatuna haja ya kuanguka katika majaribu hayo. Ni jambo muhimu kwetu kufanya maamuzi ya kupunguza majaribu maishani mwetu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake katika Mathayo 26:41, "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu." Hatustahili tu kuomba na kuwa macho dhidi ya majaribu, bali pia tunahitaji kuyatorokea. Kamwe tusijaribu kucheza na majaribu, "Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake" (Warumi 13:14). Hebu basi jitenge na watu na adhari ambazo zinafungua milango ya majaribu maishani mwako. Badala yake fanya uamuzi wa kuishi kwa uangalifu, nayo neema ya Mungu itakuwezesha kusimama dhidi ya majaribu. Lakini ukikosa kuwa makini na kufanya maamuzi ya kuruhusu dhambi kuingia ndani yako, utapata kwamba neema ya Mungu haifanyi kazi maishani mwako, kwa maana neema hiyo imedunishwa na maamuzi uliyofanya.

## Idumishe Dhamira Safi

Mtu anapookoka kwa mara ya kwanza, yeye anastahili kufanya malipo kwa watu wale ambao alikuwa amewakosea, kwa kufuata mfano wa Zakayo katika Luka 19:8-9. Lakini Wakristo pia wanahitaji kufuata mfano wa Mtume Paulo wa kila siku kudumisha maisha yao yakiwa wazi kwa Mungu na kwa wanadamu. "Nami ninajizoeza katika neno hili niwe na dhamiri isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu siku zote" (Matendo 24:16). Wakati makosa yamefanyika na unapungukiwa na ukamilifu wa tunda la Roho, hebu kuwa mwepesi kunyenyekeza moyo wako na kukiri upungufu huo wako. Jambo hili hutilia nguvu ukuaji wako wa kiroho wakati unapodumisha ushuhuda ambao uko dhahiri.

## Jifunze Kutoka kwa Biblia

Ni jambo muhimu kabisa kwa ukuaji wa kiroho Mkristo kuwa makini kusoma Biblia kila siku. "Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili

yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu" (1 Petro 2:2). Tutawezaje kujua jinsi ya kumpendeza Bwana kama hatutumii wakati wetu kusoma maneno yake kwa ajili yetu? Biblia ni Neno la Mungu ambalo tumepewa kwa ajili ya "Mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (2 Timotheo 3:16-17). Kuna sauti nyingi ambazo zinapatikana katika ulimwengu wa kidini, ndiposa ni jambo muhimu kwetu kujifunza kutoka kwa kiini cha ukweli wote, na kutafakari juu yake. Kama Daudi alivyosema katika Zaburi 119:105, "Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu."

## Sema na Mungu

Maombi ni moja ya funguo muhimu sana ya kupata baraka na ushindi wa kiroho. Je, tunastahili kuomba mara ngapi? "Ombeni bila kukoma" (1 Wathesalonike 5:17). Basi hebu tenga wakati mahsusi wa kumwomba Baba yako wa Mbinguni. Omba hapo asubuhi na mapema, kabla ya kupatana na majaribu ya maisha ya siku hiyo. Omba kabla ya kulala usiku, ili uwe na mwelekeo na moyo wa ushirika na Bwana kila wakati. Mungu ni rafiki yetu, ambaye huchukua mizigo yetu, msaidizi wetu na mfariji, kiongozi wetu. Hebu basi fungua moyo wako ili uwe na mawasiliano ya wazi na Mungu. Mungu ametega sikio lake kwetu, na Yeye ametupatia mweke wa kumwomba. "Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu" (Wafilipi 4:6). Basi unapomwona Mkristo ambaye maisha yake ya kiroho yameingia udhaifu na hata kuingia kutu, jua kwamba maisha ya maombi ya Mkristo huyo yamekuwa hafifu.

## Shiriki na Wakristo Wale Wengine

Kujitenga kiroho kumekuwa chanzo cha vifo vingi vya watoto wa Mungu. Ushirika na watakatifu wale wengine ni jambo muhimu, ndiposa ni muhimu sana waumini wapya wapate mahali pa ushirika, mahali ambako ukweli unafundishwa na watu wa hapo wanaishi kulingana na ukweli. Ni bora zaidi kuishi mahali pasipopendeza sana au hata kulipwa mshahara mdogo, lakini uwe na ushirika na waumini wale wengine kila wiki, badala ya wewe kuwa umetengwa mbali na Wakristo wale wengine na kupata kushindwa na adhari za ulimwengu. Jambo kama hili limefanyika kwa watu wengi, na hata kwa wale ambao wameoana majuzi. Jambo hili ndilo limetiliwa mkazo katika Waebrania 10:25, "Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia." Je, wewe umepatia nafsi yako umuhimu gani maishani mwako? Basi usidharau ibada na ushirika na Wakristo wale wengine.

## Shiriki Ushuhuda Wako

Funguo zingine za ushindi wa kiroho ni kushiriki ushuhuda wako na watu wale wengine. Wakristo wa mwanzo walimshindi Ibilisi "kwa neno la ushuhuda wao" (Ufunuo 12:11). Tunaposhiriki yale ambayo tumepitia kibinafsi kwa watu wale wengine, inakuwa huu sio tu ushuhuda kwa ulimwengu, bali pia ni jambo ambalo linatilia nguvu imani yetu na kutusaidia kupambana na lawama ambazo tunaletewa na adui yetu. Hili ni jambo linalotupatia nguvu za kiroho. Kamwe hatustahili kuionea "haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu" (Warumi 1:16). Tunaposhiriki na wale wengine kile ambacho Mungu ametufanyia kibinafsi, huwa pia tunasaidia kutimiza wajibu ambao Kristo alitupatia, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe" (Marko 16:15).

"Kujitenga kiroho kumekuwa chanzo cha vifo vingi vya watoto wa Mungu. Ushirika na watakatifu wale wengine ni jambo muhimu, ndiposa ni muhimu sana waumini wapya wapate mahali pa ushirika, mahali ambako ukweli unafundishwa na watu wa hapo wanaishi kulingana na ukweli."

## Mfanyie Mungu Kazi

Mungu hakutuokoa ili tukae kitako na kumsubiri Bwana Yesu kurudi. Katika ufalme wa Mungu kuna kazi ya kufanywa na kila mmoja wetu. Wakristo wengi wamerudi nyuma kwa sababu wamekuwa wavivu na kukosa kujishughulisha na kazi yake Bwana. Sisi "tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo" (Waefeso 2:10). Ilhali watu wa ulimwengu wanajilimbikiza hazina hapa duniani, sisi ambao tu watoto wa Mungu tunastahili "(ku)jiwekeeni hazina mbinguni" (Mathayo 6:19-20). Tutakuwa na nguvu zaidi za kiroho ikiwa tutashughulisha akili na wakati wetu kazini mwake Bwana. Mtume Paulo alitwambia kwamba tuwe "(Twa)tamani sana kuwa watu wenye karama za roho, takeni kwamba mzidi sana kuwa nazo ili kulijenga kanisa" (1 Wakorintho 14:12). Basi wewe unastahili kuwahudumia na kuwatumika watu wale wengine, ndipo hapo nawe utapata nguvu zaidi katika maisha yako ya kiroho. Kama ungependa kumwona Mkristo mnyonge na ambaye yuko hatarini, basi mtafute yule ambaye anaishi kwa ubinafsi wa manufaa yake mwenyewe, na ambaye hafanyi kazi kwa ajili ya ufalme wake Mungu.

Kuna wimbo unaosema, "Ana nguvu za kuokoa, ana nguvu za kudumisha." Ujuzi ambao Mkristo mpya hupata anapookoka ni wa ajabu, lakini muujiza mkuu zaidi ni mtu kuokoka na kuwa mwaminifu kwa Bwana. Basi hebu tuwe wenye hekima na tutumie funguo zilizotajwa hapa ili zifanye kazi yake, na ndipo hapo tutaweza kupata baraka ya kukua na kuwa na ushindi ndani yake Bwana wetu Yesu Kristo. ■

**JE, WAJUA?**

"Mtu ambaye huja madhabahuni kuokoka huwa haleti furaha kubwa kwa watu fulani, kwa sababu tumetambua kwamba, asilimia 95 kati ya watu 100 ya wanaookoka huwa hawashikamani ma maisha ya kanisa. Ukweli ni kwamba, wengi wao hata hawatafika kanisani mara ya pili." – Charles E. Hacket


Wokovu ni zaidi ya mtu kuja madhabahuni kuokoka, na ni zaidi ya uamuzi wa ghafla baada tu ya mahubiri. Wokovu ni ujuzi wa maisha ya mtu kubadilishwa kabisa kabisa, nao Wakristo wapya wanastahili kumfuata Yesu kila siku ili wasifanyike kuwa takwimu tu.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# MUNGU ATAFIKISHA KIKOMO KAZI ALIYOANZISHA

*Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.* — Wafilipi 1:6

Wakati mwenye dhambi amekuja kwa Kristo huku akiwa na moyo wenye toba, kunakuwa na furaha kuu mbinguni. Hapo ndipo ambapo Mungu huunda tena kile kilichovunjika, anatakasa mwenye dhambi, anambadilisha na kumfanya kiumbe kipya. Huu unakuwa ni ujuzi wa ajabu wa amani na furaha, wakati mwokovu huyo mpya anatembea katika maisha mapya.



Lakini ujuzi huu wa kwanza ni mwanzo tu. Baadaye kuna maisha ya kuishi, na punde si punde Mkristo huyo mpya anaanza kupambana na hali halisi ya nafsi yake, anapatwa na majaribu, na hata anaumizwa. Lakini huu sio wakati wa mwokovu huyo mpya kuachana na wokovu wake au kukata tamaa kwa mambo ya Mungu. Mkristo huyo anahitaji kujipa ujasiri na kuwa na uhakika ambao mtume Paulo alikuwa nao, "uhakika" kwamba Mungu aliyeokoa ataendeleza kazi yake na kumwezesha mtoto huyo wa Mungu kuishi maishi ya ushindi hadi wakati Yesu atakaporudi.

Mungu hakumtuma mwanawe kufa kwa ajilli ya dhambi zetu ili Yeye afanye kazi ambayo haikuwa kamili. Ukweli ni kwamba, Yesu ametupatia chote tunachohitaji ili tuweze kufaulu na kushinda shida za maisha. Mungu anajua udhaifu wetu, anajua mambo yale tunayoshindana nayo, na yale ambayo yanavutia mioyo yetu. Anajua kila chote ambacho kinatuhusu, na tunahitaji kuwa na pumziko na hakikisho kwamba Yeye yuko tayari na anaweza kutuhudumia hadi kwenye mahitaji yetu ya ndani kabisa. Yeye atatupatia nguvu za kuweza kumfuata Yesu kwa uaminifu, mpaka tuwe tayari kukutana na Yesu kwa amani hapo siku ya hukumu.

Wokovu huwa ni mpango kamili, na kazi yake Mungu huwa na mpango. Yeye hataachilia kazi ambayo ameianzisha bila kuikamilisha. Bali atatuongoza hadi tupate ukamilifu kupitia kwa kazi yake ya neema ambayo huendelezwa kwa nguvu zake Roho Mtakatifu. Mungu anafahamu vizuri uwanadamu wetu, na ametutolea mahitaji yetu ya kiroho ili tuweze kupata ushindi. Hatuna shida au mikazano ambayo ni mikubwa sana kumshinda Mungu. Basi hata ingawa sisi tuna uwezo wa kumwacha Mungu, Yeye kamwe hatatuacha au kusema kwamba hatujui wakati ambapo sisi tungali tumedumisha lengo letu la kumfuata Yeye. Kama hatutamuacha Mungu, Yeye pia kamwe hatatuacha.

Kusema kweli Mungu atamaliza kazi ambayo ameanzisha maishani mwako ewe Mkristo! ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA